


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# HOTUBA YA MHE. DEOGRATIUS NDEJEMBI, MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI WA MUUNGANO WA TANZANIA KWENYE UFUNGUZI WA MKUTANO WA WANAWAKE WA JUKWAA LA MABUNGE LA MKUTANO WA KIMATAIFA WA KANDA YA MAZIWA MAKUU

**UKUMBI WA KIMATAIFA WA MIKUTANO WA JULIUS NYERERE**
**DAR ES SALAAM, TANZANIA**
**2 NOVEMBA, 2026**

- ***Mhe. Adao Francisco Correia de Almeida, Rais wa FP-ICGLR na Spika wa Bunge la Kitaifa la Jamhuri ya Angola;***
- ***Mhe. Mussa Azzan Zungu, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyeji wa Mkutano huu;***
- ***Mhe. Judith Suminwa Tuluka, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo;***
- ***Wahe. Maspika na Naibu Maspika wanachama wa FP-ICGLR;***
- ***Wahe. Wabunge wa Jukwaa la Mabunge ya FP-ICGLR;***
- ***Wahe. Mawaziri wote mliopo;***
- ***Mhe. Huang Xia, Mjumbe Maalum wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa katika Ukanda wa Maziwa Makuu;***
- ***Mhe. Balozi Liberata Mulamula Mjumbe Maalum wa Umoja wa Afrika (AU) kuhusu Wanawake, Amani na Usalama;***
- ***Mhe. Dkt. Mubita Luwabelwa, Katibu Mkuu Mtendaji wa Mkutano wa Kimataifa kuhusu Ukanda wa Maziwa Makuu;***
- ***Mhe. Balozi Dkt. Deo Mwapinga, Katibu Mkuu wa FP-ICGLR;***
- ***Ndg. Baraka Leonard, Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;***
- ***Waheshimiwa Mabalozi na Wakuu wa Misheni za Kidiplomasia;***
- ***Washirika wa Maendeleo mliopo;***
- ***Wawakilishi wa Asasi za Kiraia;***
- ***Waandishi wa Habari;***
- ***Mabibi na Mabwana;***

***Habari za asubuhi!***

Kwa niaba ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, napenda kuwakaribisha nchini washiriki wote wa Mkutano huu. Namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kunipa heshima ya kumwakilisha kwenye ufunguzi wa Mkutano wa Kimataifa wa Wanawake wa Jukwaa la Mabunge la Ukanda wa Maziwa Makuu (ICGLR). Napenda pia kuwashukuru waandaaji wa Mkutano huu kwa kumwalika

Mheshimiwa Rais kuwa Mgeni Rasmi katika ufunguzi. Lakini kutokana na mwingiliano wa majukumu, Mheshimiwa Rais hakuweza kujumuika nanyi. Hata hivyo, anawatakia Mkutano mwema na wenye mafanikio.

***Waheshimiwa Viongozi na Ndugu washiriki;***

Mkutano huu pamoja na ajenda zake ni kielelezo cha jitihada kubwa zinazofanywa kuwainua wanawake na nafasi yao muhimu katika kuimarisha uongozi, kudumisha amani na kuchochea maendeleo endelevu. Kwa njia hii mnaithibitishia dunia kwamba wanawake ni kiungo muhimu katika kufikia maendeleo ya kweli na jumuishi wanaposhirikishwa katika michakato ya maamuzi na ujenzi wa Taifa. Pia, ni kudhihirisha dhamira ya kuendeleza misingi ya mshikamano, usawa na ushirikiano wa Kiafrika, ambayo imekuwa sehemu muhimu ya historia ya Bara la Afrika.

Sote tunatambua kuwa amani na usalama ni msingi wa maendeleo, na kwamba maendeleo huchochea amani na usalama. Pale kunapokosekana amani na usalama, shughuli za kiuchumi huathirika, huduma za kijamii hudhoofika na wananchi, hususan wanawake na watoto, hulipa gharama kubwa zaidi. Kwa msingi huo, wajibu wetu usiwe kusubiri migogoro itokee ndipo tuanze kutafuta suluhu, bali kuzuia migogoro na kujenga mifumo inayolinda utu, haki na usalama wa kila mmoja.

***Waheshimiwa Viongozi na Ndugu washiriki;***

Kama ilivyoelezwa, Mkutano wa Kimataifa wa Ukanda wa Maziwa Makuu ni jukwaa muhimu la ushirikiano wa kikanda lililoanzishwa kwa dhamira ya kutafuta suluhu za pamoja na za kudumu kwa changamoto zinazokabili eneo letu, hususan ukosefu wa amani, usalama, na utulivu. Jitihada hizi zinasukumwa zaidi na ukweli kwamba changamoto zinazovuka mipaka haziwezi kutatuliwa na nchi moja pekee, bali kwa ushirikiano, mshikamano, na mazungumzo ya mara kwa mara.

Historia ya jukwaa hili inatukumbusha nafasi ya kipekee ya Tanzania katika kuhimiza mshikamano na ushirikiano wa kikanda. Mnamo mwezi

Novemba mwaka 2004, Tanzania iliwakutanisha Wakuu wa Nchi na Serikali kutoka Ukanda wa Maziwa Makuu katika Mkutano wa Kilele ulioweka msingi wa kupitishwa kwa Azimio la Dar es Salaam la mwaka 2004. Hatua hiyo ilifuatiwa na kupitishwa kwa Mkataba wa Usalama, Utulivu na Maendeleo katika Ukanda wa Maziwa Makuu *(Pact on Security, Stability and Development in the Great Lakes Region),* Jijini Nairobi mwaka 2006. Nyaraka hizi mbili zimekuwa nyenzo muhimu za kihistoria zilizoweka misingi ya mfumo wa ushirikiano wa kikanda katika kuimarisha amani na usalama, kukuza utawala bora na kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika Ukanda wa Maziwa Makuu.

Akifunga Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Ukanda wa Maziwa Makuu, uliofanyika jijini Dar es Salaam mwezi Novemba mwaka 2004, Hayati Benjamin William Mkapa, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alisisitiza umuhimu wa kulinda amani, na alisema yafuatayo, nanukuu:
*"Tanzania inajitolea kuwa mshirika thabiti katika kufanikisha matumaini na matarajio ya wananchi wa Ukanda wa Maziwa Makuu ya kupata amani na maendeleo. Tutafanya hivyo tukiongozwa na imani thabiti katika utu wetu na ukweli kwamba watu wote katika ukanda huu wanastahili amani, usawa, haki na ustawi. Tutajitahidi kujenga na kukuza katika ukanda wetu utamaduni wa pamoja wa uvumilivu, mazungumzo na maridhiano."* mwisho wa kunukuu.

Katika nukuu hii tunakumbushwa kuhusu dhamira ya kujenga Ukanda wa Maziwa Makuu wenye amani, usalama na maendeleo. Hivyo, tunaamini kuwa jukwaa letu litaendelea kuhuisha misingi tuliyojiwekea takriban miaka ishirini iliyopita ili kuzuia migogoro, kukabiliana na changamoto za kiusalama, kulinda amani na kuimarisha utawala bora kupitia diplomasia, mazungumzo na maridhiano. Kupitia Mkutano huu tujitathmini na kuweka mikakati madhubuti ya kuendeleza demokrasia, amani, usalama na mshikamano wa kikanda kwa manufaa ya wananchi wetu na maendeleo endelevu ya Ukanda wa Maziwa Makuu.

***Waheshimiwa Viongozi na Ndugu washiriki;***

Jukumu la kujenga Ukanda wa Maziwa Makuu wenye amani, usalama na maendeleo ni wajibu wa kila mmoja wetu. Ili kufikia azma hiyo, tunahitaji kuhakikisha kuwa wanawake wanapewa nafasi stahiki na wana shiriki kikamilifu katika uongozi, michakato ya kufanya maamuzi na jitihada mbalimbali za utatuzi na kuzuia migogoro. Nafasi yao ni zaidi ya wahanga wa migogoro, bali ni viongozi, wapatanishi, wajenzi wa amani na wadau muhimu wa maendeleo. Nafasi yao katika familia na jamii imedhihirika katika kuwasaidia walioathirika, kurejesha matumaini na kuchangia katika kujenga upya maisha ya jamii zao

Kwa kutambua mchango huo mkubwa wa wanawake, ni wakati muafaka Jukwaa hili na mengine yakajielekeza kuondoa vikwazo mbalimbali vinavyowazuia kushiriki kikamilifu katika michakato rasmi ya ujenzi wa amani na uongozi. Ni wakati muafaka kuondosha mila na desturi zisizozingatia usawa na zinazominya nafasi ya wanawake kushiriki mazungumzo, kutoa maoni na changamoto za kiuchumi na mifumo isiyowezesha ushiriki sawa. Ushiriki wenye maana wa wanawake ni sehemu ya suluhu, ni msingi wa maamuzi jumuishi na ni nyenzo muhimu ya kujenga amani ya kudumu.

Ipo mifano hai inayoonesha uwezo na mchango mkubwa wa wanawake ambayo dunia imeshuhudia. Wanawake wameonesha uwezo, maarifa, uadilifu, uongozi na uthubutu wa hali ya juu katika nyanja mbalimbali. Baadhi ya viongozi hao ni pamoja na Ellen Johnson Sirleaf, aliyekuwa Rais wa Liberia na mwanamke wa kwanza Mwafrika kuchaguliwa kuwa Rais wa nchi; Dkt. Getrude Mongella, aliyekuwa Katibu Mkuu wa Mkutano wa Nne wa Umoja wa Mataifa kuhusu Wanawake uliofanyika Beijing, na Rais wa kwanza wa Bunge la Afrika; Profesa Wangari Maathai, mwanamazingira kutoka Kenya na mshindi wa Tuzo ya Amani ya Nobel, na wengine wengi. Mifano hii ni uthibitisho wa umuhimu wa ushiriki wa wanawake na dhamira ya kuleta mabadiliko chanya katika jamii.

***Waheshimiwa Viongozi na Ndugu washiriki;***

Pamoja na hatua zilizopigwa katika kuimarisha ushiriki wa wanawake, bado takwimu zinaonesha kuwa safari ya kufikia uwakilishi wenye uwiano haijakamilika. Kwa mujibu wa takwimu za Umoja wa Mabunge Duniani *(IPU),* wanawake walikuwa na takribani asilimia 27.5 ya viti katika mabunge duniani kufikia tarehe 1 Januari 2026. Aidha, ripoti ya Umoja wa Mataifa ya mwaka 2025 kuhusu wanawake, amani na usalama ilionesha kuwa katika michakato mikuu ya amani iliyofanyika mwaka 2024, wanawake walikuwa takribani asilimia 7 ya washiriki katika nafasi za majadiliano na asilimia 14 ya wapatanishi. Takwimu hizi zinazidi kudhihirisha kuwa ushiriki wa wanawake hautoshi na tunatakiwa kutambua uwezo wa wanawake katika mazungumzo ya amani, kamati za usalama na katika utekelezaji wa sera mbalimbali. Ili kupunguza pengo la ushiriki, nchi zetu ni lazima zijenge mifumo ya kuwainua wanawake wenye uwezo, kuwapatia mafunzo yanayohitajika na kuweka mazingira ya kazi na uongozi yanayowalinda dhidi ya ubaguzi, vitisho na ukatili.

***Waheshimiwa Viongozi na Ndugu washiriki;***

Tanzania imedhamiria na imejizatiti kuhakikisha ushiriki wa wanawake katika masuala ya amani, usalama na uongozi. Kwa miongo kadhaa, Tanzania imeendelea kuweka mazingira wezeshi kwa wanawake kushiriki katika juhudi za kuimarisha amani na usalama, kikanda na kimataifa. Mfano wa dhamira ya Tanzania katika kukuza ushiriki na nafasi ya wanawake katika uongozi ni Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye ni Rais wa kwanza mwanamke wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hivyo, kuwapa wanawake fursa ya uongozi si kauli ya kisera pekee, bali ni jambo linaloweza kutekelezwa na kuleta matokeo katika ngazi ya juu kabisa ya uongozi wa nchi.

Katika kuendeleza dhamira hii, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kuchukua hatua za kuimarisha uwezeshaji wa wanawake kiuchumi, kupanua fursa na kuongeza ushiriki wao katika maendeleo ya Taifa. Kupitia mipango mbalimbali ya uwezeshaji wa wanawake kiuchumi, tunaendelea kuwaunganisha wanawake wajasiriamali, hususan wanaomiliki biashara ndogo, za kati na kubwa na

fursa za masoko, mitaji na mikopo yenye masharti nafuu. Juhudi hizi zinalenga kuwawezesha wanawake kukuza biashara zao, kuongeza kipato, kujenga uwezo wa kiuchumi na kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya familia, jamii na Taifa kwa ujumla. Pamoja na juhudi za uwezeshaji wa wanawake katika nyanja mbalimbali, Tanzania inaendelea kutekeleza dhamira na ahadi zake za kitaifa, kikanda na kimataifa kuhusu usawa wa kijinsia, amani na usalama.

Katika kutekeleza dhamira hiyo, Tanzania imepitisha Mpango wake wa kwanza wa Kitaifa wa Utekelezaji kuhusu Wanawake, Amani na Usalama *(National Action Plan on Women, Peace and Security – WPS NAP)* kwa kipindi cha mwaka 2025 hadi 2029, uliozinduliwa rasmi mwezi Agosti, 2025. Mpango huu ni hatua muhimu katika kuimarisha utekelezaji wa Azimio Na. 1325 la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kuhusu Wanawake, Amani na Usalama, pamoja na maazimio mengine yaliyofuata yanayohusiana na ajenda hii. Azimio Na. 1325 lilitambua umuhimu wa kuwashirikisha wanawake katika kuzuia migogoro, kutafuta suluhu za amani, kushiriki katika michakato ya kufanya maamuzi na kujenga upya jamii zilizoathiriwa na migogoro**.** Vilevile, Azimio hili linasisitiza wajibu wa kuwalinda wanawake na wasichana dhidi ya ukatili unaohusiana na migogoro.

***Waheshimiwa Viongozi na Ndugu washiriki;***

Dhamira ya Tanzania katika ajenda ya Wanawake, Amani na Usalama haiishii katika mipaka ya nchi yetu. Tunaamini kuwa amani na usalama wa Tanzania vina uhusiano wa karibu na amani na usalama wa nchi nyingine katika Ukanda wa Maziwa Makuu. Kwa msingi huo, Tanzania imeendelea kushiriki katika juhudi za kikanda za kuimarisha ushiriki wa wanawake katika ujenzi wa amani na utawala bora.

Katika ngazi ya Jumuiya ya Kimataifa ya Ukanda wa Maziwa Makuu *(ICGLR),* Tanzania ilishiriki kikamilifu katika kuandaa Mpango wa Pili wa Kikanda wa Utekelezaji *(Second Generation Regional Action Plan)* wa Ajenda ya Wanawake, Amani na Usalama. Mpango huu unalenga kuimarisha ushiriki wa wanawake katika michakato ya amani, usalama

na utawala bora, pamoja na kuimarisha uratibu wa utekelezaji wa ajenda hii katika nchi wanachama. Vilevile, Tanzania ilishiriki katika kuandaa Mkakati wa *ICGLR* wa Usuluhishi na Uratibu Unaohusisha Masuala ya Jinsia *(the ICGLR Gender-response Mediation and Coordination Strategey).* Mkakati huu unalenga kuhakikisha kuwa mitazamo na mahitaji ya kijinsia yanazingatiwa katika juhudi za usuluhishi, utatuzi wa migogoro, ujenzi wa amani na kuimarisha utawala bora. Hili ni muhimu kwa sababu migogoro katika Ukanda wetu ina athari tofauti kwa wanawake, wanaume, wasichana na wavulana, hivyo suluhu tunazozitafuta zinapaswa kuzingatia mahitaji na mazingira ya makundi yote.

Kwa msingi huo, napenda kutoa wito kwa nchi zote wanachama wa *ICGLR* kuendeleza au kuimarisha Mipango yao ya Kitaifa ya Utekelezaji wa Ajenda ya Wanawake, Amani na Usalama, kwa kuzingatia mazingira, changamoto na vipaumbele vya kila nchi. Wakati huohuo, tunapaswa kuimarisha uratibu wa kikanda ili kubadilishana uzoefu, kujifunza kutokana na mafanikio na changamoto na kuhakikisha kuwa hatua zinazochukuliwa katika nchi moja zinachangia kuimarisha amani na usalama katika Ukanda mzima.

***Waheshimiwa Viongozi na Ndugu washiriki;***

Mkutano huu una fursa ya kipekee ya kuyafanya mawazo, mijadala na makubaliano yetu kuwa hatua madhubuti zitakazoleta mabadiliko chanya katika Ukanda wa Maziwa Makuu. Katika muktadha huo, ningependa kutoa wito kwa Jukwaa la Wanawake la Mabunge ya *ICGLR* kuendelea kuzingatia na kusukuma mbele ajenda muhimu zifuatazo:

***Kwanza,*** kuimarisha ushiriki wa wanawake katika michakato ya kufanya maamuzi kwa kuhakikisha wanawake wanashiriki kikamilifu katika mabunge, serikali, taasisi za usalama, kamati za amani na mazungumzo ya kutafuta suluhu za migogoro.

***Pili,*** kuimarisha diplomasia ya wanawake na mifumo ya upatanishi kwa kuendeleza na kuimarisha mitandao ya wanawake wapatanishi katika ngazi za jamii, kitaifa na kikanda. Mitandao hii inaweza kuwa nyenzo

muhimu katika kuzuia migogoro mapema, kujenga mawasiliano na kuaminiana kati ya jamii na kusaidia pande zinazokinzana kupata suluhu.

***Tatu,*** kuimarisha ulinzi wa wanawake na wasichana dhidi ya ukatili kwa kushirikiana katika kuzuia ukatili wa kijinsia, kuimarisha huduma kwa waathirika na kuhakikisha kuwa waathirika wanapata msaada, haki na ulinzi wanaostahili. Sote tunawajibika kulinda utu, haki na usalama wa wanawake na wasichana.

***Nne,*** kuwekeza katika wanawake na vijana kwa kumarisha upatikanaji wa elimu, mafunzo ya ujuzi, ujasiriamali na fursa za kiuchumi. Vilevile, tuwape vijana nafasi ya kushiriki katika juhudi za kujenga amani na kuwaandaa kuwa viongozi wenye maarifa, uwezo, uzalendo na uwajibikaji. Kuwekeza kwa wanawake na vijana ni kuwekeza katika mustakabali wa amani na maendeleo ya Ukanda wetu.

***Tano,*** kuimarisha ushirikiano wa kikanda na uwajibikaji kwa kuhakikisha maazimio ya mkutano huu yanaambatana na mpango madhubuti wa utekelezaji unaobainisha shughuli zitakazotekelezwa, muda wa utekelezaji, taasisi zinazowajibika na viashiria vya kupima mafanikio. Aidha, tuweke mifumo ya pamoja ya kufuatilia utekelezaji, kutathmini maendeleo na kutoa taarifa za mara kwa mara kuhusu hatua zilizochukuliwa na changamoto za kiutendaji zinazojitokeza.

***Waheshimiwa Viongozi na Ndugu washiriki;***

Napenda kumalizia kwa kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Adão de Almeida, Rais wa Mabunge ya Ukanda wa Maziwa Makuu, kwa kuongoza kwa ustadi Jukwaa hili muhimu. Kuaminiwa kwako kushika nafasi hii ni kielelezo cha imani iliyowekwa kwako katika kuendeleza ajenda ya amani, mshikamano, demokrasia na utawala bora katika Ukanda wa Maziwa Makuu. Vilevile, nimpongeze Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuwa mwenyeji wa Mkutano huu. Aidha, nampongeza Balozi Dkt. Deo Mwapinga, Katibu Mkuu wa Jukwaa hili; Ndugu Baraka Leonard, Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; pamoja na

kamati nzima ya maandalizi kwa uratibu mzuri uliofanikisha kufanyika kwa Mkutano huu.

Mwisho, ninawasihi nyote tuungane ili turithishe vizazi vijavyo amani tuliyoijenga, mshikamano tuliouimarisha na maendeleo tuliyoyasimamia, na si migogoro tuliyoshindwa kuitatua.

Baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ninayo heshima kubwa kutamka kuwa Mkutano wa Wanawake wa Jukwaa la Mabunge la Mkutano wa Kimataifa wa Ukanda wa Maziwa Makuu *(ICGLR)* umefunguliwa rasmi.

**Mungu ibariki Tanzania**
**Mungu zibariki nchi zote za Ukanda wa Maziwa Makuu**
**Mungu ibariki Afrika**

Asanteni sana kwa kunisikiliza.